AUSCO

Programu ya Maelekezo ya Kitamaduni nchini Australia

# Maelezo ya Jumla ya Australia



## Lugha

Kiingereza ni lugha ya kitaifa ya Australia. Kujifunza Kiingereza ni muhimu kwa kutulia na kwa mafanikio katika Australia. Hata hivyo, zaidi ya lugha 200 zinazungumzwa katika nyumba na jamii kote Australia. Hii ni kwa sababu karibu asilimia 25 ya wakazi wa Australia walizaliwa katika nchi nyingine, na kuna lugha ya asili zaidi ya 20 bado inasemwa katika Australia.

## Watu wa asili wa Australia

Watu wa Asili wa Visiwani vya Torres Strait wamekuwa wakiishi katika Australia kwa karibu miaka 50,000 na ni miongoni mwa tamaduni kongwe duniani. Watu wa asili wa Australia huishi katika kila jimbo na wilaya ya Australia. Watu wa Asili wa Visiwani vya Torres Strait wa Australia wana lugha mbalimbali, imani za kitamaduni na za kiroho katika maeneo mbalimbali katika Australia.

## Australia ya utamaduni mwingi

Australia ina wahamiaji kutoka duniani kote. Tangu mwaka 1945, zaidi ya watu milioni 7.5 wamehamia Australia, ikiwa ni pamoja na wakimbizi zaidi ya 800,000.

Asilimia arubaini na sita ya watu nchini Australia walizaliwa ng'ambo au wana mzazi ambaye alizaliwa ng'ambo. Hii inafanya Australia jamii ya kitamaduni sana.

Australia haina dini rasmi au dini ya taifa. Waaustralia wote wana uhuru kufuata dini yoyote wanaochagua kama si kinyume au kuhitilafiana na sheria za Jumuiya ya Madola ya Australia (Australian Commonwealth) na za jimbo na wilaya.

Maadili ya usawa, demokrasia, uhuru na heshima kwa wote ndicho kinachounganisha Waaustralia.

Australian Government
Department of Social Services

Inaletwa kwako na Shirika la Uhamiaji la Kimataifa kwa niaba ya Idara ya Huduma za Jamii nchini Australia

IOM • OIM